**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA BARIADI**

**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA SIMIYU,**

**Anwani ya Simu:**
**MKUU WA SHULE Simu nambari: 0766854321,**
**MAKAMU MKUU WA SHULE Simu nambari: 0747025279**
**SANDUKU LA POSTA 109,**
**BARIADI-SIMIYU.**

JINA LA

MWANAFUNZI……..…………………………………………………………………

S.L.P…………………………

…………………………………

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA SIMIYU, HALMASHAURI YA WILAYA YA BARIADI MKOA WA SIMIYU MWAKA… … … . . .**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka…….. na atasoma tahasusi ya ……………. Shule ya Sekondari ya wasichana Simiyu (SIMIYU GIRLS) ipo **KIJIJI CHA IGEGU KATA YA SAPIWI** umbali wa **Kilometa 45** kutoka katika Mji wa BARIADI MJINI Usafiri wa basi kutoka mjini unapatikana katika kituo cha mabasi **Somanda Bariadi** Nauli ni Shilingi **3000.** Pia shule inapatikana umbali wa **kilometa 25** kutoka Mji mdogo wa **LAMADI** kwa nauli ya Tsh.**2000** kwa gari. Kwa maelezo zaidi piga simu elekezi hapo juu.

   Muhula wa Masomo unaanza tarehe **itakayotangazwa na Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI.**

**1.1 Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni sketi mbili (2) za drafti esteem no. 1 ndefu inagusa kisigino. Mashono ni linda boksi. (zinapatikana shule*);* **RANGI YA KITAMBAA CHA SKETI**




ii. Shati mbili aina ya tetroni mikono mirefu zisizo bana na ziwe ndefu (kama ni mwislam ashone nusu kanzu nyeupe na juba jeupe) na hijabu nyeupe za darasani kwa waislam.

iii. Sare ya Michezo ni truck suit ya Kijivu (gray) yenye michirizi myeupe 1, Tshirt ya jezi ya gray 1 na raba nyeupe wote na wachezaji wa mpira wa miguu waje na viatu vyenye meno.

iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi; Haturuhusu viatu vingine vyenye urembo wa aina yoyote.

v. Soksi jozi tano nyeupe za shule;

vi. Sweta rangi ya kijani mgomba 1. (yanapatikana shuleni)

vii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) gauni 2, rangi ya brown esteem no. 1 (Urefu ni **kuvuka magoti** kwa wakristo na kufunika miguu kwa urefu wa sentimeta 5 kwa Dini zote, mikono mifupi kwa wakristo na mirefu kwa waislam mashono ni solo na hijabu kwa waislam rangi ya brown.

viii. Tisheti (T-shirt form six) nyeupe 1 yenye kola.

### 2.2

i. Madaftari manane (8) quire 4, karamu za risasi na za wino na Mathematical set (MKEBE);

ii. **Ream (A4) doule A** Mbili (2) kwa mwaka;

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha tazama kwenye kiambata chini);*

iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;

v. Lab koti nyeupe kwa wanafunzi Wote yenye mikono mirefu na inayovuka magoti;

vi. Scientific Calculator kwa wanafunzi wote(FX 991 Old version);

vii. Godoro moja futi $2^{1/2}$ x 6 (Tan foam) lisiwe la pamba;

viii. Mashuka Jozi 2 rangi ya bluu Bahari 1 na pink 1, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 rangi nyeupe na mto 1(pia mashuka yanapatikana shuleni);

ix. Nguo za ndani za kutosha,Taulo, kitenge doti moja **(asije na kanga);**

x. Vyombo vya chakula (kontena, kikombe na kijiko pia vinapatikana maeneo karibu na shule);

xi. Ndoo 1 kubwa na ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko na dumu la lita tano la kuhifadhia maji ya kunywa;

xii. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mifagio 2 wa ndani 1 (soft bloom) na nje 1 (Hard bloom);
xiii. Aje na sabuni ya maji lita tano;
xiv. Rain boot;
xv. Chupa ya chai ya maji ya moto ya chuma; na
xvi. Picha 4 za passport size.

**2.3 Michango mbalimbali**

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Michango ilipwe kwenye account ya shule**
**JINA LA BENKI:**
**CRDB JINA LA AKAUNTI: SHULE YA SEKONDARI WASICHANA SIMIYU**
**NAMBA YA AKAUNTI: 0150855146000 (fedha hizi hazipokelewi mkononi)**

2.2 **ANGALIZO:** Fedha ya matibabu/ **Bima ya afya NHIF (Gharama yake ni 50,400/= kwa mwaka NI LAZIMA), AJE NAYO MKONONI ISILIPWE KWENYE AKAUNTI nak ama anayo BIMA ni vema aje nayo.**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

### 3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule (Njia tano au saba);
vii. Kufuga kucha;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiuakuua kama kunywa sumu; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.
xvii. Kukataa adhabu kwa makusudi.

## 4. Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;

**Angalizo: Mwanafunzi atakayebainika kudanganya vipimo vya hospitali baadae kugundulika na tatizo la muda mrefu ambalo halikubainishwa na daktari atarudishwa nyumbani.**

ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.**

**TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0766854321**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0747025279/0713393136.**
- **Mwandamizi Taaluma 0766390729**
- **Mwandamizi Malezi 0748747919**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**PRIME MINISTER’S OFFICE**

**REGIONAL ADMINSTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**SIMIYU GIRLS SECONDARY SCHOOL**
**FORM FOR MEDICAL EXAMINATION**

(TO BE COMPLETED BY MEDICAL OFFICER IN RESPECT OF ALL FORM 5 ENTRY)

**STUDENT’S FULL NAME………………………………………………………………….**

AGE………………………………………………………………….
STOOL EXAMINATION…………………………………………

BLOOD COULT RED& WHITE……………………………………

URINALYSIS……………………………………………………..

TB TEST…………………………………………………………

EYE TEST………………………………………………………….

SYPHILIS TEST……………………………………………………

CHEST……………………………………………………………

SPLEEN……………………………………………………………

ADDITIONAL INFORMATION: Eg Physical impairment(s), chronic or family diseases, Etc…………………………………………………………………….………………

………………………………………………………………………………………………

I certify that I have examined the above pupils and recommended that she is fit/unfit to pursue further education

Signed…………………………………….

Designation…………………………………

Official stamp………………………………

Date……………………………

**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA SIMIYU**

## AHADI YA MZAZI/MLEZI:

Mimi………………………………………………………………………… (Jina kamili) ambaye ni Mzazi/Mlezi wa ……………………………………………. kidato cha …………...nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa vyema,Nimekubali mwanangu ajiunge na shule hii.Naahidi kwamba nitashirikiana na uongozi wa shule katika kumpatia binti yangu malezi na elimu bora kwa manufaa ya taifa la Tanzania, Na nitatoa msaada kadri ya uwezo wangu nitakapotakiwa kufanya hivyo.Ninaahidi kwamba ninakubaliana na yote yaliyotajwa kwenye barua hii mfano sheria,kanuni na maelekezo mengine yaliyotolewa na shule.

Saini ya mzazi………………………………….

Na. ya simu……………………………………………………….

Anuani kamili……………………………………………………………

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**

**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA SIMIYU**

**AHADI YA MWANAFUNZI:**

Mimi…………………………………………………….(Jina kamili) ambaye ni mwanafunzi nimeyasoma maagizo haya na kuayaelewa,ninakubali nafasi nilyopewa ya kujiunga na shule hii. Ninaelewa kuwa nafasi hii ni dhamana, hivyo ninaahidi mbele ya wazazi/ walezi wangu kwamba nitatumia nafasi hii kwa kushirikiana na uongozi wa shule kutimiza na kutekeleza yale yote yaliyo katika maagizo haya.Nitatii na kufuata sheria za shule wakati wote.

Saini ya mwanafunzi…………………………………………….

Jina kamili………………………………………………………

Shahidi…………………………………………………………

Jina kamili………………………………………………………

Saini…………………………………………………………….

Tarehe…………………………………………………………

**HALMASHAURI YA WILAYA YA BARIADI SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA SIMIYU**
**FOMU YA HISTORIA YA MWANAFUNZI.**

**1.**JINA LMWANAFUNZI**…………………………………………………………………….**

**2.**JINA LA MZAZI/MLEZI WMWANAFUNZI………………………………………………

3.JINA LA SHULE ANAKOTOKA……………………………………………………….

4.TAREHE YA KUZALIWA…………………………………………………………….

5.KATA ANAYOTOKA MWANAFUNZI……………………………………………………

6.WILAYA ANAYOTOKA MWANAFUNZI…………………………………………………

7.MKOA ANAOTOKA MWANAFUNZI……………………………………………………..

8.KABILA……………………………………………………………………………….

9.URAIA………………………………………………………………………………..

10.DINI/DHEHEBU……………………………………………………………………

11.ANUANI YA MZAZI/MLEZI……………………………………………………….

12.NAMBA YA SIMU YA MZAZI/MLEZI NYUMBANI……………………………………..

OFISINI……………………………………….. E-MAIL…………………………………...

ADRESS……………………………………………………………………………

ANUANI YA POSTA KWA AJILI YA KUTUMA MATOKEO YA MTIHANI

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

**13. MAJINA MANNE YA NDUGU WA KARIBU WALIOIDHINISHWA KUCHUKUA NAFASI YA MZAZI/MLEZI ENDAPO DHARULA ITATOKEA**:

| No. | JINA | **UHUSIANO** | SEHEMU ANAKOISHI | NAMBA YA SIMU |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |
| 4 | | | | |

## BAADHI YA VITABU VYA A-LEVEL AMBAVYO MZAZI/MLEZI ANAWEZA KUMNUNULIA MTOTO/MWANAFUNZI

**PHYSICS**

1. Nelkon and parker
2. Understanding physics
3. Rodger Mancaster
4. Calculation for A-level
5. Martha, R& Martha, V.K (2009). Principle of physics for class xi. S. Chand and Company ltd. New Delhi

**ADVANCED MATHEMATICS**

1. Advanced Mathematics for Secondary Schools Student’s Book Form 5&6 T.I.E (2022)
2. Pure mathematics 1 & 2 Backhouse
3. Pure mathematics vol 1 & 2 S. Chand
4. Understanding mathematics
5. Statistics for A level
6. Engineering mathematics
7. Septine silem, A level mathematics form five and six
8. Advanced Mathematics (**Tranta**)

**CHEMISTRY**

1. Freementle M. Chemistry in action. Macmillan education ltd 3rd edition.
2. Advanced chemistry anna and Patrick
3. Advanced chemistry (S. Chand). BIOLOGY 1. Biological science (Bs) 3rd edition
4. Understanding biology 3rd Edition
5. Biology for advanced level secondary school (TIE) student book



**MWL. HURUMA A. MTINDYA**
**MKUU WA SHULE**

HEADMISTRESS
SIMIYU GIRLS SEC. SCHOOL
P.O. BOX
BARIADI